

**JIMBO KATOLIKI LA MOROGORO**  
**ALFAGEMS SECONDARY SCHOOL (S. 3874)**  
**P.O.Box 6083 – Morogoro**

Simu: 0689-783630 (Ofisi Taaluma) / 0685-701614 (Ofisi Uhasibu)  
0689-783672 (Bweni la Kike) / 0689-782670 (Bweni la Kiume)  
0789-978886 (Airtel Money)  
www.alfashule.ac.tz / www.alfagems.com

**TARATIBU ZA KUJIANDAA KWA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA KWA MWAKA MMOJA**

Ndugu ....., tunafurahi kukujulisha umepata nafasi ya kujiunga na masomo ya kujiandaa mwaka mmoja kwa mtihani wa kidato cha sita kwenye shule yetu iliyoko katika manispaa ya Morogoro, kata ya Tungi, mtaa wa Mji Mwema (kati ya Msamvu na Nanenane). Karibu sana!

**Ada ni:**

- (a) Kwa mwanafunzi wa kutwa Tsh. 600,000 kwa mwaka. Inalipwa kwa mkupuo mmoja.
- (b) Kwa msichana wa bweni Tsh. 1,400,000 kwa mwaka. Unaruhusiwa kulipa kwa mikupuo minne, yaani Tsh. 800,000 ule wa kwanza, halafu 200,000 mara tatu kabla ya kila nusu mhula. Bweni la wavulana halina nafasi.

Kwa usalama wa wote unaombwa **ulipie benki** (akaunti yenye jina la shule iko CRDB, namba 0152077746000), si kwa mawakala wao wala kwa simu, **halafu vocha uilete shuleni** katika ofisi ya mhasibu upate risiti yetu. Nje ya hapo usitoe pesa kwa yeyote, hata kama ni mwalimu wetu: malipo ya namna hiyo si halali, hivyo shule haihusiki nayo. Jihadhari sana!

Shule imekubaliwa pia kuwa wakala wa kampuni ya Airtel Money kwa ajili ya kutuma pesa kwa urahisi zaidi. Namba ni 0789-978886 na inatumika kwa mawasiliano na kwa kutuma pesa.

Bila ya kutimiza malipo yote yanayotakiwa hutapokewa. Tena ukichelewa kujisajili kwa malipo utakosa nafasi yako.

Masomo yataanza tarehe 20-5-2025.

(a) Ukitaka kuwa mwanafunzi wa kutwa ufike shuleni tarehe hiyo saa 8:00 mchana. Ukichelewa wiki moja kuripoti na kuleta vocha ya benki nafasi yako anaweza akapewa mwingine.

(b) Ukitaka kukaa bweni ufike kabla ya saa 10:00 jioni ya tarehe iliyotangulia mwanzo wa masomo (kwa kuwa nafasi hazitoshi kwa wote, watapewa wasichana waliowahi kuleta vocha ya benki hata kabla ya tarehe hiyo).

Ulete Biblia (isipokuwa kama si Mkristo), kamusi ya Kiingereza na vitu vilivyoorodheshwa hapa chini:

1. Sare kama ifuatavyo (huruhusiwi kuleta nguo za aina nyingine):

(a) Kwa wasichana:

- (i) Fulana ya buluu yenye maandishi ya shule
- (ii) Sketi ya rangi ya damu ya mzee (ifikie sentimeta 20 kutoka ardhini)
- (iii) Viatu vyeusi visivyo na visigino virefu
- (iv) Soksi nyeupe zisizo na urembo wowote
- (v) Sweta ya rangi ya damu ya mzee
- (vi) Masista wanaruhusiwa kuvaa sare ya shirika

(b) Kwa wavulana:

- (i) Fulana ya buluu yenye maandishi ya shule
- (ii) Suruali ya rangi ya damu ya mzee
- (iii) Viatu vyeusi visivyo na visigino virefu
- (iv) Soksi nyeupe zisizo na urembo wowote
- (v) Sweta ya rangi ya damu ya mzee
- (vi) Mabradha wanaruhusiwa kuvaa sare ya shirika.

2. Kwa kukaa bweni (wasichana tu):

- (a) Fulana ya kijani yenye maandishi ya shule
- (b) Nguo ya kulalia na ya kwenda bafuni
- (c) Mashuka na blanketi
- (d) Chandarua kilichotiwa dawa
- (e) Godoro la futi mbili unusu
- (f) Ndoo
- (g) Sanduku imara na salama
- (h) Taulo na vifaa vingine vya usafi
- (i) Sahani, bakuli, kikombe na kijiko
- (j) Nauli ya kurudia nyumbani wakati wowote (ukibaki wakati wa likizo utalipa Tsh. 2,000 kwa siku).

**N.B. Ni lazima** mashati, fulana za shule, sketi, suruali, sweta na taulo za kike vinunuliwe shuleni.

Biblia (Tsh. 22,000), kamusi (Tsh. 22,000), godoro (Tsh. 42,000), blanketi (Tsh. 15,000), shuka (Tsh. 7,000), chandarua (Tsh. 6,000), trakisuti (Tsh. 20,000), taulo (Tsh. 6,000), ndoo (Tsh. 4,000), begi (Tsh. 20,000), viatu (Tsh. 27,000 visipozidi namba 42), daftari na kalamu vinapatikana shuleni kwa bei nafuu kama ilivyoonyeshwa katika mabano.